# Jazanda na Utambulisho wa Kijamii katika Tawasifu: Mfano wa Riwaya za *Unbowed, A Memoir* (Wangari Maathai) na *Nasikia Sauti ya Mama* (Ken Walibora)

*Ombito Elizabeth Khalili*
*Chuo Kikuu cha Rongo, Kenya*

**Ikisiri**

**Riwaya ya tawasifu ni kitengo kisicho na maandishi mengi ya Kiswahili nchini Kenya kama ilivyo tawasifu katika lugha ya Kiingereza. Upekee wa tawasifu ni masimulizi ya mwandishi mwenyewe kujihusu kimaisha kwa lengo la kuuleza ukweli wake binafsi kisanii. Aghalabu, mtunzi wa tawasifu huteuwa yale anayotaka kutambulishwa nayo au kujulikana kwayo kati ya matukio na tajiriba zake nyingi za maisha. Hivyo basi, masimulizi mengi kwenye tawasifu humwelekeza msomaji kumtambua mwandishi kindakindaki kupitia kwa usemi wake mwandishi mwenyewe. Tabia, hulka, imani, matamanio na mazoea huungana kuijenga falsafa ya mwandishi wa tawasifu, ambayo huwa kichocheo kikubwa kwenye uandishi wake; yaani kujitambulisha binafsi na jamii yake. Ni muhimu kwa mtunzi wa tawasifu kuteuwa matukio, wahusika, mbinu na maudhui yanayomjenga yeye na kuitambulisha jamii yake kitabia, kitamaduni na kifalsafa. Mojawapo ya mbinu za kisanii zinazotumika kujieleza kifalsafa ni jazanda. Makala haya yanajadili matumizi ya jazanda kama kipengele cha utambulisho wa kijamii kwenye riwaya za kitawasifu kwa mintaarafu ya nadharia ya semiotiki.**

**Maneno Muhimu:** Jazanda, Utambulisho, Tawasifu, Jamii.

## Utangulizi

Ufasili wa tawasifu unafungamana sana na mtindo wa mwandishi binafsi. Sababu ni kwamba mtunzi wa aina hii ya riwaya hupata fursa ya kuelezea maisha, historia, ilhamu, falsafa na matamanio yake kisanii, jinsi apendavyo. Aghalabu, mtunzi huteuwa mandhari, matukio, wahusika na mbinu kimaksudi yanayoafiki hisia, matendo na wakati ili kufanikisha maudhui yake kwa msomaji. Uumbuji wa kisanii humpa mtunzi wa nathari uhuru wa kuteuwa mbinu faafu za kimtindo ili kujieleza kwa kina. Makala haya yanalinganisha upekee wa kimtindo kati ya waandishi Wangari Maathai na Ken Walibora, hasa namna wanavyotumia mbinu ya jazanda kujieleza kihulka, kifalsafa na kimtazamo kupitia tawasifu ya

*Unbowed: A memoir* (Maathai, 2007) na *Nasikia Sauti ya Mama* (Walibora, 2014). Mjadala unatathmini namna ambayo jazanda imetumika kukuza sifa ya mwingilianomatini kama kipengele cha nadharia ya semiotiki kwenye riwaya ya tawasifu.

Nimeteuwa riwaya ya *Unbowed: A memoir* iliyoandikwa na Wangari Maathai ambaye alikuwa msomi maarufu wa Bayolojia na masuala ya mazingira, ili kuilinganisha na ile ya *Nasikia Sauti ya Mama* iliyotungwa na Ken Walibora, msomi na mwandishi wa lugha na fasihi ya Kiswahili. Waandishi hawa wameishi katika mazingira yanayolingana na kusomea nchini Kenya na Marekani kwa nyakati tofauti. Licha ya Maathai kuandika riwaya yake katika Kimombo na Walibora kutumia lugha ya Kiswahili, kuna mshabaha wa kimtindo na kinadharia katika tawasifu zao unaozitambulisha jamii zao? Sehemu ya kwanza ya makala inaangazia utunzi wa tawasifu na umuhimu wake katika fasihi ya Kiswahili. Katika sehemu ya pili, misingi ya nadharia ya semiotiki inajadiliwa mintaarafu ufasili wa tawasifu. Sehemu ya tatu ya makala inatathmini mtagusano wa mbinu ya jazanda, falsafa za watunzi na utambulisho wa kijamii kwenye tawasifu za *Unbowed: A memoir* na *Nasikia Sauti ya Mama*.

## Tawasifu

Madumulla (2009) anafafanua tawasifu kuwa nathari inayohusu maisha ya mtunzi mwenyewe. Mwandishi wa tawasifu hujisimulia maisha ya utotoni, utu uzima na matarajio yake ya baadaye kwa njia ya safari, huku akitaja matukio aliyokutana nayo na athari za matukio hayo kwa mtazamo wake maishani. Utungo huu hushabihi sana historia ya mwandishi kutokana na ukweli wa matukio anayochagua kuyasimulia. Kutokana na desturi ya tawasifu kuandikwa kwa kufuata maisha ya mtu binafsi kuanzia utotoni hadi uzeeni, mtunzi huangazia maisha yake katika vipindi vyake vya ukuaji kwa kujumuisha tarehe kamili za matukio (Bengtsson, Ovesen na Fity, 2008). Hata hivyo, mtunzi wa tawasifu ana uhuru wa kuchagua matukio anayotaka kujinasibisha nayo kwa masimulizi. Aghalabu tawasifu hutungwa na watu mashuhuri katika jamii kama vile wanasiasa, wasomi au mashujaa wasifika wanaotaka kusimulia hadithi yao wenyewe ili isomwe na hadhira kama kumbukumbu kuwahusu. Pili, mwandishi wa tawasifu hunuia kujenga hulka ya kibinafsi kupitia kujitathmini na kujichunguza kimaisha ili kubaini mchango wake kwa jamii. Hivi ni kusema kwamba, mwandishi wa tawasifu kupenda kujitambulisha mwenyewe kwa hadhira kwa njia iliyo wazi kwa kuwapa wasomaji sababu maalum za kuyasoma masimulizi ya historia yake (Bengtsson, Ovesen na Fity, 2008). Wakati mwingine, mtunzi hulenga kusahihisha mtazamo potovu wa jamii kumhusu kwa kujisimulia mwenyewe kimaandishi.

Hata hivyo, kitengo cha tawasifu kina ukuruba mkubwa na memwa (*Memoir*) ambayo hasa hutungwa na mwanasiasa kusimulia juhudi zake za kisiasa kuliko

maisha yake ya faragha (Smith, Sidonie na Watson, 2001). Wangari Maathai ni mwanamke wa Kiafrika aliyetambuliwa ulimwenguni kote kama msomi, mwanaharakati wa kutetea na kuhifadhi mazingira; mpiganiaji wa demokrasia na haki za wanawake nchini Kenya. Kujitambulisha kwa riwaya yake na memwa kulichochewa na azma ya kujitambulisha kwa walimwengu kuwa alikuwa na usuhuba mkubwa na maumbile, mali asili na mtagusano uliopo kati ya binadamu na mazingira yake. Huenda Maathai alichagua kuandika kwa lugha ya Kiingereza ili riwaya yake isomwe na wengi. Hivyo basi, tungo ya *Unbowed, A Memoir* ina ugiligili wa tawasifu na memwa kwa sababu ni rekodi ya harakati za kupigana vita dhidi ya ukoloni, ukoloni mamboleo, pamoja na kutamauka kwa Mwafrika wa ngazi ya chini kulikosababishwa na ubinafsi na unafiki wa viongozi weusi (Alabi, 1998). Riwaya ya *Unbowed, A Memoir* ni masimulizi yanayomsawiri Maathai katika jamii, mwanamke wa Kiafrika katika jamii ya kabila la Wagikuyu, wakazi wa kijiji cha Ihithe, katika Kaunti ya Nyeri, nchini Kenya. Licha ya kusimulia zaidi kuhusu mafanikio yake kielimu, kiuchumi na kijamii, mtunzi wa memwa hujifunga mkanda mmoja na jamii yake, akajitokeza kuwa kioo cha jamii husika. Maathai amesimulia pakubwa mila, desturi na imani za Wagikuyu zinazofungamana na uhifadhi wa mazingira, kwa kutumia jazanda zinazojenga taswira ya uhalisia wa mandhari yao katika kipindi maalum cha kihistoria.

Ken Walibora ni mwanamume wa kiafrika anayetambulika ulimwenguni kama mtangazaji wa habari, msomi, mwalimu na mwandishi wa fasihi ya Kiswahili. Tawasifu ya *Nasikia Sauti ya Mama* ni mdokezo wa maisha ya kifaragha na uhusiano wake na jamaa yake wakati wa utotoni. Kwa maneno yake mwenyewe azma ya kutunga tawasifu hiyo ilikuwa ni kujitambulisha mwenyewe kwa hadhira ya waliomfahamu hasa kutokana na kutamba kwa jina lake ila wasiujue usuli wake na misukosuko iliyomkuza na kumfikisha alipo ukubwani. Kinyume na Maathai, tawasifu ya Walibora inachukuwa mkabala wa kihistoria ambao unahusisha fasihi na jamii alimokulia mwandishi na namna ambavyo mwandishi amekuwa jinsi alivyo kutokana na taathira za kijamii (Msokile, 1983). Je, kuna uhusiano wa kimtindo unaoitambulisha jamii ya watunzi hawa kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki katika ya tawasifu ya *Nasikia Sauti ya mama* na *Unbowed: A memoir*?

## Nadharia ya Semiotiki kwa Ufasili wa Riwaya

Mhakiki anayegemea kwa nadharia ya semiotiki hulenga kuainisha na kufafanua maana za ishara za kisanii alizotumia mwandishi katika ubunifu wake. Wasemavyo Wafula na Njogu (2007: 103), semiotiki ni "Taaluma ya mipangilio ya ishara inayomwezesha binadamu kuona vitu au hali kama ishara zenye maana." Ishara zinazotumika katika tungo ya fasihi huelezwa kwa misingi ya utamaduni wa jamii fulani inayozipa maana pana. Asemavyo Eagleton (1996), ishara kwenye tungo ya fasihi zinaweza kuwa vitu vya kawaida vipatikanavyo kwenye mazingira halisi kama vile milio ya ndege, taa za trafiki au ishara

zinazopatikana katika hospitali. Ishara hizo zinaweza kutumika kisanii na kuchukua maana pana inayoeleweka na wazungumzaji wa lugha husika. Msomaji wa tawasifu hana budi kuingiliana pakubwa na mila, desturi na miiko ya wazungumzaji wa lugha ya mwandishi ili kuufasili ubunifu wa mwandishi mwenyewe. Suala la muktadha wa masimulizi hutawala ufafanuzi wa ishara za kifasihi kwa mujibu wa wanasemiotiki. Katika sura hii, ishara za kisanii kwenye tawasifu zinachukuliwa kuwa mbinu ya jazanda. Kwa maoni ya Wamitila (2008) jazanda zinaweza pia kuwa za kimaelezo au za kimaelezi au za kiishara. Ishara na maelezo hayo hubeba maana inayochangia kunatisha ujumbe wa mtunzi kwa akili za msomaji kwa kumwezesha kujenga taswira ya hulka na falsafa ya mwandishi. Wangari Maathai ameteuwa ishara zinazosawiri mandhari yanayoeleza misitu, maeneo ya mashambani, kilimo na bustani za maeneo ya mijini nchini Kenya na Marekani. Walibora naye ametumia jazanda ya sauti kujieleza kifalsafa.

**Jazanda kwenye Tawasifu**

Ili kujitambulisha kijinsia, Maathai anapanga faharasa ya riwaya ya *Unbowed, A memoir* kulisawiri umbo la mwanamke. Taswira inayojitokeza ni:

*CONTENTS*

*Acknowledgements xi*

*1. Beginnings 3*

*2. Cultivation 29*

*3. Education and the State of Emergency 53*

*4. American Dream 73*

*5. Independence – Kenya's and My Own 98*

*6. Foresters Without Diplomas 119*

*7. Difficult Years 139*

*8. Seeds of Change 164*

*9. Fighting for Freedom 184*

*10. Freedom Turns a Corner 206*

*11. Aluta Continua: The Struggle Continues 230*

*12. Opening the Gates of Politics 254*

*13. Rise Up and Walk 277*

*Epilogue: Canopy of Hope 291*

*Appendix:*

*Konyeki na ithe, or "Konyeki and His Father" 297*

*Index 305*

(Maathai, 2007)

Ishara inayoashiriwa inaweza pia kumaanisha mti mkubwa, uliokuwa katika mazingira ya mwituni ambao matawi yake hayakuwahi kupogolewa. Jazanda inayojitokeza ni mwanamke anayeienzi na kuihifadhi miti katika mazingira yake halisi bila kuuathiri ukuaji wake. Katika riwaya, Maathai anachukuwa miaka mingi kutafitia kupe anaowapata mwituni kwa stashahada ya utabibu wa mifugo, aliyosomea kwenye Chuo Kikuu cha Nairobi. Mti uliokomaa bila matawi yake kupogolewa pia ni jazanda inayomsawiri Wangari Maathai kama mwanamke asiyemruhusu yeyote hasa mwanamume, kiongozi, nguvu za kiutawala au usomi kumkengeusha kutokana na asili yake.

**Jazanda ya Mti**

Taswira ya mti mkomavu inamwelekeza msomaji kwa methali ya Kiswahili isemayo 'Mti unyooshe ungali mchanga.' Katika jamii za Kiafrika, malezi ya watoto yalikuwa juhudi za jamii nzima. Watu wazima, hasa wazazi walishauriwa kuwaadabisha watoto watukutu ili kuwaelekeza kuwa wenye maadili na tabia njema. Adabu ya Kiafrika mara nyingi ilijumuisha kuwachapa watoto waliokosa nidhamu, kuwakaripia na pia kuwashauri. Kwa kutumia mti mkomavu wenye umbo la mwanamke, Wangari Maathai anazikejeli juhudi za utawala wa rais Moi na chama cha KANU pamoja na Mwangi, aliyekuwa mumewe, za kutaka kumwadhibu ukubwani ili kumfanya atii wanaume na kuwa mwanamke aliyeitikia kihewala sheria na tamaduni potovu. Rais Moi alitumia nguvu za mahakama na askari kumtia Maathai korokoroni alipopinga ujenzi wa jumba la kifahari la *Times Media Complex* katika Bustani la Uhuru, alipopinga unyakuzi wa ardhi ya Msitu wa Karura na aliposhirikiana na kina mama wenzake kushinikiza serikali kuwaachilia huru wafungwa wa kisiasa.

Miti imetumika kuonyesha uharibifu wa ardhi ya Mwafrika nchini Kenya. Walipokuja walowezi wa Kiingereza nchini Kenya, waling'oa miti ya kiasili iliyokuwa imenawiri na kupanda miti ya kigeni iliyokua upesi. Aina mpya ya miti kama vile Miwati na Mikalatusi ilikuzwa kwa wingi licha ya kuwa iliathiri chemchemi za mito. Si miti ya kigeni tu iliyokuzwa na Wazungu, bali mikahawa na michai ilipandwa kwa hamasa na Waafrika waliotarajia mapato kutokana na mauzo ya kahawa na chai. Maathai anasistiza umuhimu wa miti asili, hasa Mitini kwa kusema: "Mitini ilichukuliwa kuwa miti ya Mungu. Sisi [Wagikuyu] hatuikati, wala hatuichomi." (Maathai, 2007, uk. 45) [Tafsiri yangu]

Mtini unatumiwa kujenga taswira ya makazi salama kwa ndege kutokana na kanopi yake nzito. Si uhai wa ndege tu uliosetiriwa na mtini, bali uhai wa wanyama na wanadamu wote kupitia kuwepo kwa chemchemi ya mto kando ya mti wenyewe. Mtunzi anaelezea mandhari hayo kwa kusema kuwa:

> Umbali wa takriban yadi mia moja kutoka pahali ulipokuwa mti [mtini] palikuwa na kijito kilichoitwa Kanunga, chenye maji yaliyokuwa safi na baridi tuliyokunywa moja kwa moja kutoka kwenye kijito…Pale

> palipokuwa na chemchemi palikuzwa magimbi, na kando ya kijito, palikuzwa migomba ya ndizi na miwa; vyakula vya kiasili…kuliponyesha, matone ya mvua yaliyochukuwa rangi ya fedha yalichezacheza na kudondoka kitaratibu kwenye majani ya mimea hiyo kabla ya kuanguka mchangani. Tulitumia majani hayo ya magimbi kuteka maji ya kijito na kuyanywa" (Maathai, 2007 uk. 45) [Tafsiri yangu]

Katika mandhari hayo, mtunzi anachora taswira ya mtoto aliyetegemea kijito Kanunga kwa maji safi ya kunywa, na kwa upande mwingine taswira ya kijito Kanunga kutegemea kuwepo kwa mti wa Mtini kama chanzo chake. Si ajabu basi Mtini unapokatwa na nafasi yake kuchukuliwa na mikahawa, maji ya kijito Kanunga yanapungua na upana wa kijito hicho kupungua vilevile. Mtunzi anazilaumu juhudi za walowezi wa Kizungu za kuwahimiza Wagikuyu kukata miti ya kiasili bila kukadiria athari zake kwa chemchemi za mito. Jazanda ya Mtini inasawiri mandhari ya kiishara yanayoashiria uhai wa binadamu unaotegemea sana maji.

Hata hivyo, Maathai anahimiza ubora wa miti ijapokuwa ya kigeni, kama hifadhi ya wanyama pori na binadamu. Anasimulia kisa kimoja kilichotokea wakati wa vita vya *Maumau* nchini Kenya katika miaka ya 1950. Alikuwa akiishi na binamuye aliyeitwa Wangari kijijini Ihithe. Usiku mmoja, mamake Wangari aliwatanabahisha kuwa wanamgambo wa Maumau walikuwa wamelivamia boma lao. Wasichana hao walifichwa kwenye kichaka cha miwati wakiwa na kitoto kichanga kilichokuwa kimelala fo fo fo. Katika hofu ya kushikwa mateka, wasichana hao walianza kukariri rozari kwa imani ya kujiokoa. Muujiza ukatokea walipomwona chui akijipitia kando asiwaone wala kuwashambulia (Maathai, 2007: 65). Msimulizi anahusisha kunusurika kwake usiku huo na kule kujificha kwenye kichaka cha miti. Katika riwaya, mtunzi alielezea etimolojia ya jina la Wangari kuwa lenye maana sawa na mnyama chui. Ni sadfa kuwa chui mnyama mwitu anawapita mtunzi na binamuye aliye somo wake bila kuwadhuru kwa sababu somo hao watatu walikuwa katika mandhari asilia ya wanyama (msituni). Tukio hili linadhihirisha ukweli wa imani za Wagikuyu kuwa chui hawezi kumdhuru chui mwenzake. Wasemavyo wahenga 'Chui ana wakwe pia'. Haya ni mandhari ya kidokezi, yanayouweka msingi wa kitamaduni katika fasili na uchanganuzi wa tawasifu (Wamitila, 2008). Utamaduni wa Wagikuyu ulizungumzia usuhuba kati ya wanyama mwitu na binadamu, hasa kwa wakazi wa Ihithe, eneo lililo karibu na Mlima Kenya ambao uliwasetiri wanyama pori wa aina nyingi.

Kwa mwanamazingira kama Wangari Maathai, miti ilikuwa jazanda ya kuashiria binadamu mashujaa walioenziwa na jamii. Shirika la *Green Belt* lilipanda miti saba ya kiasili katika uga wa Kamukunji jijini Nairobi tarehe 5, mwezi Juni, 1977. Miti hiyo ilipandwa baada ya maandamano ya kuadhimisha

Siku Kuu ya Mazingira ulimwenguni. Miti saba ilipandwa kiishara kuwakilisha mashujaa kutoka makabila tofauti ya Kenya kama vile marehemu: Wangu wa Makeri aliyekuwa chifu wa kike kutoka eneo la Murang'a kabla ya ukoloni; chifu Waiyaki wa Hinga, aliyesalitiwa na Kapteni Fredrick Lugard miaka ya 1890; Bi Mekatilili wa Menza mtawala wa kike aliyeongoza kabila la Wagiryama kupigana vita dhidi ya wakoloni nchini Kenya, chifu Masaku Ngei wa kabila la Wakamba; chifu Nabongo Mumia wa Himaya ya pekee kihistoria ya Wawanga; chifu ole Lenana wa kabila la Wamaasai na Gor Mahia, kiongozi shupavu na shujaa wa kivita wa kabila la Wajaluo (Maathai, 2007 : 131-132). Ingawa mashujaa hao waliwahi kuishi na kuenziwa na jamii zao, mtunzi anawachagua kimaksuudi kuwasilisha falsafa yake kuhusu demokrasia na utaifa wa Kenya.

Miti hiyo saba ilipaswa kuonya serikali ya Moi kuwa Kenya ilikuwa ya makabila yote na usawa wa kijinsia ulikuwa haki ya kila mmoja. Jazanda hii pia inadokeza waigwa wa mtunzi kama vile Wangu wa Makeri na Bi Mekatilili wa Menza. Ujumbe anaouhimiza mtunzi ni kuwa mwanamke hafai kudharauliwa kutokana na jinsia yake kwa sababu anacho kipawa cha uongozi sawa na mwanamume. Kumithilishwa kwa viongozi wa kike na miti katika historia ya Kenya kunaibua kumbukumbu za mapambano makali ya vita dhidi ya ukoloni hasa vita vya Wagiryama na Wagikuyu ambapo wanawake walichukua nafasi ya mbele kuwahamasisha wapiganaji kwa kuwalisha viapo vya kidini ili kuwamotisha. Vilevile katika riwaya ya *Unbowed, A memoir*, Maathai anajitokeza kuwa kiongozi shupavu anayeongoza wanawake kuupinga unyakuzi wa ardhi na utawala wa kimabavu wa rais Moi. Juhudi zake zinatambuliwa ulimwenguni kote anapotuzwa tuzo la Amani la Nobel mwaka wa 2004 na kuingia kwenye historia kuwa mwanamke wa kwanza Barani Afrika kupewa tuzo hilo.

Uhusiano wa miti na amani unaelezwa bayana na Maathai anapotumia jazanda ya mti kuonyesha taswira ya binadamu wa tabaka la chini na wale wa tabaka la juu. Anasema hivi:

> Ingawa mti una mizizi yake ardhini, hukua ukielekea mbinguni. Mti hutuambia kuwa hata binadamu akwee juu vipi kimamlaka, daima mizizi yake itarutubishwa na ardhi. Ukweli huu ni ukumbusho kwetu sisi tuliopata mafanikio maishani kuwa tusije tukasahau asili yetu. Funzo kuu ni kuwa hata tuwe na vyeo vikubwa serikalini, au tupate tuzo nyingi maishani, mamlaka, nguvu na uwezo wetu wa kufikia malengo yetu huwategemea watu, hasa wale walio mashinani; watu ambao kazi zao hazitambuliwi, watu wanaomithilishwa na ardhi inayotukuza sisi na inayotubeba mabegani." (Maathai, 2007 uk. 293) [Tafsiri yangu]

Jazanda hii inaonyesha kuwa binadamu hutegemea jamii yake jinsi mti utegemeavyo ardhi kuuhimili licha ya uzito na urefu wake. Jamii inaweza

kuchukuliwa kama taifa linalompa mtu uraia na utambulisho wake. Miti imesawiriwa kuwa chombo mahsusi cha mawasiliano kati ya wanyonge na watawala. Mtunzi anaeleza jinsi wanawake walivyopanda miche ya miti mbele ya lango la kuingia kwenye Msitu wa Karura hasa walipozuiliwa kuingia msituni kwa nia ya kupinga unyakuzi wa ardhi. Ingawa walinda usalama waliing'oa miche hiyo pindi ilipopandwa, wanahabari walichapisha picha za wanawake hao magazetini wakipanda miti ili kuufikisha ujumbe huo kwa watawala. Pia Maathai binafsi aliyazuru maeneo yaliyokumbwa na vita vya kikabila katika eneo la Bonde la Ufa nchini Kenya ili kuwatuliza mioyo wale waliofurushwa kisiasa kutoka kwa mashamba yao ili wasilipize kisasi. Katika ziara zake za kuhubiri amani na upatanisho, Maathai aliwapa miche ya amani ili waikuze na kusameheana.

**Jazanda ya Mito**

Mbali na miti, mtunzi anatumia jazanda ya mto Chania kusawiri safari yake ya kielimu iliyompeleka katika misheni ya Tetu, mbali sana na kijiji cha Ihithe, safari iliyochukuwa siku mbili huku akiwa amelibeba sanduku la mbao mgongoni. Anasimulia kwa utondoti taswira ya kuuvuka mto Chania kwa kusema:

> Mto ulirunguruma kwa povu jingi huku maji yakitiririka kusini mwa bonde. Mimea mingi ilizifunika kingo za mto na hewa katika sehemu hiyo ilikuwa nzito na yenye unyevu. Chini yangu,[nilikuwa kwa kidaraja cha waendao kwa miguu] mto ulichukuwa rangi ya weusi huku ukitoa povu, na nilikuwa na hofu ningetumbukia majini ikiwa ningetazama mawimbi ya kutisha yaliyopita majini…Hivyo basi niliangaza macho yangu mbele kutazama ukingo wa pili wa mto hadi nikauvuka." (Maathai, 2007:55) [Tafsiriyangu].

Kivukio cha waendao kwa miguu kinaonyesha taswira ya hofu kwa msichana mdogo aliye pweke na aliyeubeba mkoba mgongoni akisafiri kutafuta elimu. Haya ni mandhari ya kidokezi yanayomdokezea mwandishi kuhusu hali ngumu ya safari ya kupata elimu hasa kwa mtoto wa kike. Kidaraja kibovu juu ya mto wenye mawimbi makali yatishayo ni dalili ya mkondo mgumu wa maisha yanayomsubiri Maathai shuleni na hasa katika siku za usoni. Kule kukaza macho upande wa pili wa mto Chania ni ishara ya kujikaza kisabuni, kuvumilia na kutunga makini kwa kile alichojitolea kufanya. Kuvuka daraja lile ni ishara ya ufanisi masomoni ambao mtunzi aliupata katika viwango vyote vya masomo kutokana na bidii na kujitoloea kwake. Mandhari haya si mageni katika maeneo ya mashambani nchini Kenya, hasa kwa mtoto wa kike. Licha ya ugumu wa safari ya elimu kwa mtoto wa kike, Maathai aliweka historia kuwa mwanamke wa kwanza barani Afrika kupata shahada ya uzamivu.

Jazanda ya mto inajitokeza tena kuueleza uhusiano wa Maathai na shirika la *Green Belt*. Analiita shirika hilo 'Mto Mkuu' ambao huanza kwa chemchemi ndogo itokayo kwenye ufa ardhini mithili ya kijito Kanunga kijijini Ihithe. Hata hivyo, mto huundwa kutokana na vijito vingine vinvyoungana ili maji yake yatiririke kwa mkondo mmoja mkubwa. Mtunzi anaainisha vijito vitatu vilivyokuwa vyanzo vya dhana ya *Green Belt* maishani mwake. Kwanza ni kule kuteuliwa kuhudumu kwa Bodi ya shirika la *Environment Liaison Centre* kama mwakilishi wa Waafrika. Majukumu yake kwenye shirika hilo yaliwiana vema na mazingira ya kijijini Ihithe alikolelewa akifahamu vema uhusiano kati ya binadamu na mazingira walimoishi. Kijito cha pili ni tajiriba yake ya utafiti kuhusu kupe waliosababisha ndwele kwa mifugo ilimfahamisha mengi kuhusu uharibifu wa mazingira uliosababisha mmomonyoko wa ardhi na uchafuzi wa maji ya mito. Kijito cha tatu ni kule kuwa mwanachama wa muda mrefu wa shirika la *National Council of Women of Kenya* (NCWK). Shirika hilo liliwaunganisha wanawake kupitia vikundi vyao mbalimbali waliokutana kujadili hali zao kimaisha. Wasilisho la mtafiti mmojawapo wa kike kuhusu hali ya utapiamlo miongoni mwa watoto katika eneo la kati nchini Kenya walikoishi Wagikuyu kwa wingi; kutokana na ukuzaji wa mimea ya kuuzwa, lilimzindua Maathai na kumtia mshawasha wa kulibuni na kuliendeleza shirika la *Green Belt* kwa upanzi wa miti.

**Jazanda ya Wanyama**

Mandhari ya misitu yamekoleza taswira ya uhai wa binadamu, ndege na pia wanyama. Mtunzi anazungumzia wanyama wa kufugwa na wale wa mwitu ili kukamilisha mtagusano wa binadamu na mazingira yake. Memwa hujumuisha visasili vya jamii ya mwandishi kama kiunzi cha fasihi na utamaduni wake. Maathai anafafanua usuli wa jina la 'Wangari' kuwa lenye kumaanisha mnyama Chui katika desturi za Wagikuyu. Anamnukuu mvyele wake akimwambia kuwa "Ukiwa watembea njiani na uuone mkia wa chui…jihadhari usiukanyage. Badala yake, endelea kutembea na umwambie yule chui kuwa 'Mimi na wewe ni chui, hivi kwa nini tusielewane?" (Maathai, uk. 43) [Tafsiri yangu]

Mtunzi anasimulia matendo katika maisha yake yanayomithilishwa na tabia za mnyama chui. Kihulka, chui ni mnyama anayehofiwa na binadamu kwa kuwa hachelei kuwaangamiza na kuwala. Kitabia, Maathai ni mkakamavu, asiyetishwa na serikali wala nguvu za kiutawala, hadi apate haki anayoidai. Mandhari ya wanyama pori yangalipo na hulitambulisha taifa la Kenya kama kivutio kwa watalii kote ulimwenguni.

Punda anatumiwa na mwandishi kubeba maharagwe yenye uzito unaomlemea hasa apitapo kwenye vilima vya Ihithe akiandamana na Maathai. Jazanda ya punda inaashiria nguvu za mtunzi hasa asemapo kuwa hata naye alibeba nusu gunia la maharagwe mabichi aliyokuwa amevuna mgongoni mwake

na kumfuata punda aliyebeba gunia zima za maharagwe mgongoni mwake. Wawili hao wanapofika nyumbani, wanaiangusha mizigo hiyo mizito kwa uchovu mwingi. Katika riwaya, mtunzi anasimulia kuhusu nguvu zake za ujanani na jinsi zilivyomwezesha kulima kijishamba chake, kukuza miti na kuwahamasisha wanawake kukuza miti mashambani mwao katika sehemu nyingi za Kenya.

Jazanda ya zimwi liitwalo Konyeki inasimuliwa na mtunzi kupitia ngano. Katika fasihi simulizi ya Wagikuyu, ngano ya *Konyeki na Ithe* ilihusu zimwi lililomvutia msichana mrembo hadi akaamua kuolewa kwalo, licha ya makanyo mengi kutoka kwa dada zake. Yule msichana alimzaa mwana wa zimwi aliyewala watu kama Konyeki. Hatimaye mazimwi yale yanapomla dadake, mwanamke yule anatumia ujanja kuyaua mazimwi na kujinusuru pamoja na wana mapacha waliokuwa tumboni mwa marehemu dadake. Katika riwaya ya *Unbowed, A memoir*, mazimwi yanawakilisha utawala wa viongozi dhalimu, wenye lengo la kuangamiza wachochole. Viongozi hao hupora na kuharibu maliasili kwa manufaa yao wenyewe kwa kuwapumbaza raia wao. Mwisho wa mauti kwa *Konyeki na Ithe* kunaonyesha utabiri wa ukombozi wa jamii inayodhulumiwa. Kuwa, siku moja, mnyonge ataerevuka ajiopoe ma dhuluma za wenye nguvu; hata kama mnyonge na mwenye nguvu wana unasaba. Harakati za yule mwanamke zinachangia kueleza hulka ya Maathai kisiasa nchini Kenya.

Ndovu ametajwa kwenye masimulizi ya Maathai kuwa mnyama aliyegadhabishwa na wanakijiji hadi akauliwa na walinzi wake. Ili kudumisha muamana kati ya wanyama mwitu na binadamu, shirika la *Kenya Wildlife Service* lilitenga uga uliotumiwa kama njia ya ndovu walipotembea kati ya Mlima Kenya na Aberdares. Siku ya kuuliwa kwa ndovu hao, walikuwa wamepotea njia wakapita katika mashamba ya wenyeji waliowafukuza kwa kelele nyingi. Ndovu anawakilisha uhalisia wa maumbile. Kuwa, ni lazima binadamu, aliye na akili zake akubali kuishi na wanyama pori kwa kuwatengea nafasi yao katika mazingira. Nafasi hiyo inaponyakuliwa na kutumiwa kwa kilimo au makazi, wanyama mwitu huathirika na mwishowe huvamia mashamba ya binadamu na kuleta madhara. Kifo cha ndovu ni jazanda ya kuzorota kwa uchumi wa nchi kutokana na uharibifu wa mazingira; jambo ambalo Maathai alisimama kidete kulipinga maishani.

**Jazanda ya Bustani**

Mandhari ya *The English Garden*, katika jiji la Munich yalimtuliza moyo Maathai na rafikize. Anaeleza bustani hilo kuwa lenye mandhari ya kupendeza asemapo kuwa:

> Nilipenda jiji la Munich na hasa niliyafurahia mandhari ya bustani la *The English Garden*…Bustani hilo ndilo kubwa zaidi Bara Uropa, lenye urefu wa maili mbili u nusu mraba, na lapatikana mkabala na Mto Isar. Majira

> ya kipupwe, bustani hilo hujaa maua yenye rangi za kupendeza, miti yenye majani mabichi na nyuga pana. Majira ya kuanguka kwa barafu tulifurahia kutembelea bustani hilo na hasa kuona barafu na kuufaidi utulivu wake."(Maathai, 2007:108) [Tafsiri yangu]

Mwandishi anasimulia mandhari ya Munich ili kumpa msomaji taswira ya kihisia kuhusu uchukivu alioupata alipoambiwa kuwa bustani la *Uhuru Park* jijini Nairobi lingenyakuliwa na walowezi kwa ujenzi wa jumba la *Times Media Complex*. Ujenzi wa jengo hilo ungewahini wanyonge fursa ya kujivinjari bustanini. Analiita jengo hilo 'Zimwi la bustanini'.

**Jazanda ya Jangwa**

Mwandishi anasimulia kuhusu jangwa la Sahara kwa hisia za masikitiko kwa namna alivyolishuhudia. Katika usimulizi wa nafsi ya kwanza, mtunzi anaieleza taswira ya jangwa kwa kusema kuwa:

> Nililitazama jangwa jua lilipochomoza, nikapatwa na usingizi kisha nikaamka masaa mengi baadaye na kuzidi kuona wingi wa mchanga…Ndege ilikuwa inapaa juu zaidi nisiweze kumtambua mwanadamu wala mnyama ardhini. Ardhi iliyokuwa chini yetu ilirembwa maumbo ya kuajabisha ya vilima vya mchanga na kitone kimoja kimoja cha kijani kibichi kilichoashiria chemchemi ya maji jangwani (Maathai, 2007: 75). [Tafisri yangu]

Uchukivu wa mwandishi kwa Jangwa la Sahara ulikuwa msukumo mkubwa kwake katika kutetea uhifadhi wa mazingira kwa matumizi ya vizazi vya sasa na vya baadaye. Jazanda ya jangwa inarejela ukame kwenye nia za walionyakua misitu ya umma na kung'oa miti ili kujenga makazi, jambo ambalo hatimaye lingesababisha ukame nchini Kenya.

Kinyume na jangwa, mtunzi anasimulia jazanda ya Mlima Kenya ili kujenga hisia ya furaha kuushangilia ushindi wa Tuzo la *Nobel* kwa kuyahifadhi mazingira. Tukio la kuutazama Mlima Kenya linaibua utamaduni wa mtunzi anayejitambulisha na kabila la Wagikuyu. Katika desturi za Wagikuyu, Mlima Kenya ni makazi ya Mungu wao na wana uhusiano wa kibinadamu na mlima huo. Maelezo yafuatayo yanathibitisha madai haya:

> Mlima [Kenya] unafahamika kuwa wenye uoga, aghalabu, kilele chake hufunikwa kwa kofia ya mawingu…Ingawa nilikokuwa miale ya jua ilikuwa ya mwangaza mpevu, mlima ulikuwa umeuficha uso wake. Nilipoutafuta uso huo kwa macho na moyo wangu, nilikumbuka jinsi nilivyouhofia uhai wa mlima huo dhidi ya uharibifu tulioutendea sisi binadamu. Kadri nilivyozidi kuutafuta uso adimu wa mlima huo, ndipo nilipoamini kuwa mlima ulikuwa umeungana nami kusherehekea. Kamati ya Nobel ilikuwa imeisikiliza sauti ya maumbile, tena kwa njia mahsusi kabisa. Nilipomtazama mrembo huyo, nilihisi kuwa hata naye

> huenda alikuwa akilia machozi ya furaha, ingawa kayaficha kwenye mawingu meupe yaliyomfunika. Wakati huo, nilihisi nimesimama kwenye ardhi takatifu (Maathai, 2007, uk. 293). [Tafsiri yangu].

Masimulizi haya yanajenga taswira ya mlima kama mama mpole aliyewabariki na kuwazingira wanawe kwa hali na mali. Unasaba wa mwandishi na mlima unaonyesha utamaduni aliouenzi na hasa mshikamano uliokuwepo kati ya binadamu na mandhari alimozaliwa na kulelewa. Mlima pia ni jazanda ya ugumu wa maisha ya Maathai hasa katika harakati za kuyatetea mazingira dhidi ya kuharibiwa na watawala nchini Kenya. Ufanisi wa juhudi zake unaashiria kuwa japo kusimamia na kutetea haki kuna miinuko mingi, kujitolea kwake hatimaye kulitambulika ulimwenguni kote. Mlima huu pia unatumika kulitambulisha taifa la Kenya.

Ndoto ya Maathai kuhusu maisha ya baadaye ni kuwa na jamii inayotawaliwa kidemokrasia ambapo haki za binadamu, mazingira pamoja na tamaduni chanya zenye kulinda rasilmali zinaenziwa. Anatumia jazanda ya kigoda cha utawala wa Kiafrika chenye viguu vitatu (Maathai, 2007:294). Kila kiguu cha kigoda hicho kinawakilisha ukweli fulani. Kiguu cha kwanza, kinasimamia nafasi ya kidemokrasia kama vile kuheshimu haki za binadamu na za kimazingira. Kigoda cha pili kinasimamia ugavi sawa, usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za nchi kwa raia. Nacho kiguu cha tatu kinaashiria uzingativu wa mila na desturi za kulinda amani kati ya binadamu na mazingira yake. Kikalio cha kigoda kinawakilisha jamii ya Kiafrika na matarajio ya maendeleo yake kwa ulimwengu wa sasa. Taswira hii inaonyesha kuwa ukamilifu wa binadamu katika mandhari yake ni juhudi za kimakusudi ambazo zinahitaji maamuzi ya busara hasa miongoni mwa watawala na sio tamaa na ubinafsi wa kupora rasilmali za umma. Usawa na haki ni kaulimbiu ya mtunzi katika maisha yake.

Falsafa kuu ya Wangari Maathai inafungamana na juhudi zake za kuweka mazingira nadhifu. Anaamini kuwa lipitalo hupishwa hasa likiwa lenye kumkera na kumzuia asiifuate ndoto yake ya kukuza miti. Ndoa yake kwa Mwangi ilitibuka siku ile Mwangi alipofunganya virago vyake na kuihama nyumba walimokuwa wakiishi. Maathai anapogundua kuwa mumewe kamwacha, anachukuwa ufagio na kufagia nyumba nzima. Hisia ya kufagia inamvaa ghafla:

> Fagia ! nafsi yangu ikaniamuru. Nilitii hiyo amri na nikaelekea jikoni, kuuchukua ufagio na kuanza kuufagia uchafu aliouacha Mwangi. Nilifagia jikoni, nikaelekea sebuleni, hadi kwenye chumba cha kulala. Nilifagia ushoroba hadi mlangoni, nikafika hadi nje. Nilifagia vumbi lililoachwa wazi na Mwangi alipopakia mizigo yake…Nilipofagia chembe ya mwisho ya vumbi, nilifanya mkataba moyoni mwangu kuwa nitakubali hatima ya ndoa hii… (Maathai, 2007: 141-142) [Tafsiri yangu]

Jazanda ya ufagio na vumbi vinashiria mwanzo mpya katika maisha ya Maathai. Vumbi linaashiria ukame unaoletwa na talaka ilhali ufagio unaashiria juhudi za kuanza upya maisha kwenye mazingira safi yasiyo na bughudha za mume. Falsafa hii ilidumishwa na mtunzi kwa sababu hakuingia tena kwenye ndoa na mume mwingine wala kurudiana na Mwangi bali aliishi maisha yake akiendeleza kazi zake kwa heshima na ukomavu. Maathai ametumia mbinu ya jazanda kufafanua falsafa na hulka yake kama mwanamazingira, mwanasiasa, msomi na mtetezi wa wanyonge.

## Jazanda za Sauti katika *Nasikia Sauti ya Mama*

Nadharia ya semiotiki, kwa mujibu wa Ferdinand de Saussure na Charles Pierce, inasistiza umatini na hasa mwingilianomatini (Wamitila 2006:132-136) kati ya tungo. Kwamba, tungo yoyote ile haiwezi kusimama pekee yake bila kuwepo na vipengele vya mshabaha na tungo za awali au za baadaye. Mwingiliano huo unaweza kuwa wa kimaudhui, kimtindo, kifalsafa, au kimaudhui. Mwingiliano unaoangaziwa katika makala haya ni wa kimtindo baina ya waandishi Wangari Maathai na Ken Walibora katika tawasifu zao. Maathai amejitambulisha zaidi kupitia jazanda za ishara. Upande wa pili wa jazanda ni jazanda za kimaelezo, hasa matumizi ya sauti kama mtindo wa kuwasilisha falsafa na hulka ya mtunzi Ken Walibora.

## Sauti ya Simiyu

Salamu kati ya Walibora na rafikiye wa zamani Simiyu zilibaini ukweli kuwa licha ya kuwa Walibora alikuwa mtangazaji mtajika, aliyesikika Kenya nzima kwenye redio na kushabikiwa na wengi, rafikiye wa karibu hakujua alikokuwa akifanya kazi wala kazi aliyokuwa akiifanya. Kutokuwa na mwao kumhusu rafiki wa dhati kulizindua Walibora kutambua kuwa kunao wengi waliojidai kumjua ilhali hawakumfahamu alikuwa nani na usuli wake ni upi. Sauti hiyo ilimchochea kujieleza mwenyewe kupitia tawasifu yake ili kuwafanya wanaomshabikia na kumwajabia kuwa mtu aliyezaliwa na rundo la vipawa kufahamu unyonge wake maishani. Falsafa yake kuu imefumbatwa kwenye imani kuwa "…katika ushinde na uhange na udhalili, na utundu na uzuzu wa maisha yangu ya utotoni, kuna vilevile cheche na chachu za matumaini ya ushindi na uungwana, na werevu" (Walibora, 2014: viii). Walibora anaamini kuwa maisha yake ya awali yalisheheni kweli-kinzani ambayo isingenga'muliwa upesi na wale waliomjua tu kutokana na umaarufu wake ukubwani, hadi awaeleze kwa kinywa chake mwenyewe. Safari ya maisha yake inafumbwa kwenye kitangulizi cha tawasifu yake, dondoo la shairi la Wasakatonge lililotungwa naye Muhammed Seif Khatib. Ubeti huo unaelezea shangilio la Walibora kuwa japo amepitia bahari yenye wingi wa mawimbi na misukosuko kimaisha, hakuangamia bali alifika ufukweni akiwa taabani.

### Sauti ya Malkia Maube na Mariamu

Mwanzoni mwa tawasifu, Walibora anasimulia mapokezi yake kwa sauti ya Malkia Maube, mwanafunzi wa kike waliyesoma naye katika shule ya msingi ya St. Joseph's na bintiye mwalimu jirani yao. Malkia aliinyakua ripoti yake Walibora na kuangua kicheko cha kumbeza kwa kukokota mkia darasani ilhali alikuwa mwanawe mwalimu mkuu wa shule ya msingi ya St. Joseph's. Sauti hiyo inaashiria gere waliokuwa nayo wanafunzi mahasimu wa Walibora kwa kumtarajia kuwa mwanafunzi mwerevu darasani hasa katika shule iliyoongozwa na babake mzazi. Sauti hii ya bezo inajitokeza kwenye wahusika wengine wa kike waliombeza Walibora shuleni na nyumbani; isipokuwa mamake mzazi. Kwa mfano Mariamu, yaya wao alimtolea maneno ya dhihaka kwa kumtaka Walibora amwonyeshe kwa macho kama kweli *kachongwa kalamu* au yungali kabeba filimbi kwenye nyeti zake (uk. 29). Sauti hii ilipokelewa kama shinikizo la kujaribisha maonjo kwa asali ile aliyokuwa kakanywa na mamake kuwa ni halali tu ya watu wazima. Sadfa ni kuwa sauti ya Malkia na ile ya Mariamu ni vicheko vilivyomdhalilisha na kumtahayarisha Walibora.

### Sauti ya Babu Makali

Walibora anakinasibisha kipawa chake cha sauti ya utangazaji na urithi alioupata kutoka kwa babu Makali. Anasema kuwa walioujua usuli wake walidai kuwa katunukiwa kumrithi mzee huyo kwa sauti ambayo ilimfaa sana kuwa mtangazaji redioni. Hata hivyo, licha ya babu yake kuwa mlokole aliyehubiri kanisani, palizuka tukio la kuyaokoa mahindi ya jirani kwa kuwaondoa ng'ombe shambani liliomfanya mzee huyo kushukiwa kuwa mwizi na kupigwa kibuhuti. Asemavyo nyanyake Walibora:

> Babu yako alijaribu kuwambia kwamba yeye si mwizi ila kajitolea sabili kuwaondoa mifugo shambani wasiyamalize mahindi ya watu. Ila nani amsikilize? Nani amwamini? (Walibora, 2014 : 37).

Tukio hilo la kupigwa kwa babuye Walibora ni jazanda inayoonyesha ukweli-kinzani katika jamii. Kwamba, licha ya yeye Walibora kuwa na sauti pendezi kwenye redio na runinga, inayoshabihi ile ya babu yake, na fauka ya sauti ile ile ya babu kuwaliwaza watu kwa mistari ya Biblia kanisani, hakuna aliyetaka kuisikiliza tena aliposhukiwa kimakosa kuwa mwizi wa ng'ombe. Jazanda hii inashadidia falsafa ya Walibora kuwa walimwengu hawana jema; hujitia kumsifu mtu ilhali wamwonea gere pakubwa na hutabasamu ilhali nyoyo zao zikimuwazia mtu mabaya. Hata hivyo, msimamo wake ni ule wa mamake kuwa ni vema mwanadamu kutenda wema kwa vyovyote vile. Sadfa ni kuwa aliyepiga kamsa kuwatanabahisha majirani ni mwanamke.

### Sauti ya Bibi Sara Kusimba

Hii ndiyo sauti aliyoipenda sana Walibora kwa kumtumbuiza na kumpatisha tasnifu za fasihi simulizi ya jamii yake. Masimulizi ya bibi yalimjengea msingi

thabiti wa kuwa msemaji bora, mwanafasihi na mwandishi maarufu baadaye. Kupitia masimulizi ya bibi, Walibora alielezwa kuhusu ukoo wake na maisha yao ya awali, mila zao, miiko, amali na miviga yao. Mwandishi analinganisha sauti ya bibi na ile ya mwalimu wake maarufu, mama yake. Bibi aliposimulia ngano ya Kasuku, alimzingatisha pia fomyula za kuanza na kukamilisha ngano, pamoja na kumwimbia wimbo wa njiwa. Walibora anakiri kuwa kweli ngano zilitekeleza majukumu maalum kama vile kufunza maadili mema, kuburudisha, kuonya, kuunganisha vizazi vya kale na vya kisasa pamoja na kuliwaza. Liwazo la ngano linasistizwa kwa maneno haya:

> Katika pandashuka za maisha yetu utotoni, katika nenda rudi, katika mapatano na mapatilizano ya maisha, na katika afua na athari za maradhi hasa yale yaliyomfuma mama kifai, ngano za bibi zilikuwa chanzo mahsusi cha faraja na tiba ya moyoni. Kana kwamba alitupaka mafuta mororo kwenye nyuso zetu zilizoyabisika. (Walibora, 2014:10).

Sauti ya bibi ni mafundisho yaliyoijenga tabia ya Walibora ya kuwa mtunzi na msimulizi maarufu wa tungo za fasihi. Ithibati katika tungo zake za riwaya hasa *Siku Njema, Ndoto ya Almasi, Siku Njema* na *Nasikia Sauti ya Mama* ni matumizi ya nyimbo na mashairi mafupi mafupi ambayo ni mbinu ya kujenga mtagusano kati ya kipera cha fasihi simulizi na fasihi andishi. Kupitia kwa sauti ya bibi, tunajuzwa kuhusu imani ya kabila la Wabukusu iliyotokana na fomyula ya ngano kuwa mtoto akihitimisha ngano kwa fomyula ya bibi au mtoto mwenzke, basi angedumaa. Hii ni kanuni ya urejelezi wa viashiria vya utamaduni wa jamii husika unaohusisha vitu fulani vinavyotajwa kwenye masimulizi na utamaduni anaoweza kujitambulisha nao msomaji wa kazi ya fasihi (Wamitila 2006:134). Dhima kubwa ya fasihi simulizi ilikuwa ni kuhifadhi na kukuza utamaduni wa jamii kutoka kizazi hadi kingine ili kuielekeza vilivyo. Katika tawasifu ya *Nasikia Sauti ya Mama*, Walibora anatutajia majina ya ng'ombe wao waliofugwa sehemu za mashambani kule Cherengani. Ng'ombe hao waliitwa majina ya Kibukusu yaliyoashiria maumbile, ukoo au walikotoka. Mwandishi anataja majina kama: Nasikumu (mkosa pembe kichwani); Kusimba (bibi yake wa kumeni); na Munyinyi (aliyenunuliwa kwa mkulima tajiri aliyeitwa Munyinyi).

### Sauti ya Baba Mzazi

Ni sauti iliyomlea na kumfunza Walibora kuenzi tabia ya upole na kushabikia lugha ya Kiswahili maishani. Hii ndiyo sauti inayojitokeza kuingiza lugha ya Kiswahili katika mtaala wa elimu ya shule ya msingi kinyume na sera ya lugha nchini Kenya kwa wakati huo. Juhudi za babake Walibora zinaelezwa bayana kuwa:

> Sijui kwa nini baba alisistiza kukiporomosha Kiswahili kwenye gwaride na hata kukifundisha Kiswahili. Kiswahili halikuwa somo la kutahiniwa

> kwenye mtihani wa taifa wa darasa la saba Cerificate of Primary Education (CPE). Sijui hadi leo kama baba na naibu wake waliufuata mtaala wa Wizara ya Elimu au walijiundia mtaala wao wenyewe. Hata hivyo, hapana shaka kwamba wakati wizara ilipozuumu kujenga na kuwaumba vijana kama Wazungu kasoro ngozi, Waafrika wanaochukia kuwa Waafrika, wanaochukia lugha zao, wanaochukia majina yao na asili yao, baba na naibu wake walikuwa wanaelekeza kwenye fahari na nemsi ya lugha ya Kiswahili. (Walibora, 2014: 75).

Juhudi za kuzungumza na kuwafunza wanafunzi wa shule ya msingi Kiswahili ni jazanda ya kuzindua vipawa miongoni mwa watoto kwa kuwazingatisha lugha na fasihi ya Kiafrika shuleni. Sauti nyingine ya Kiswahili ilitoka kwa Kuto, kakake Walibora. Baada ya kujiunga na shule ya upili ya Kenya High School kule Mwatate, alirejea nyumbani akitema Kiswahili kwa lafudhi ya kipwani, ambayo ilimvutia sana Walibora kuwa msomi na mwandishi wa Kiswahili baadaye. Sauti hiyo uya Kuto ilimtumbukiza Walibora kwenye ulingo wa ushairi na kupalilia kipawa chake cha kutunga kazi za fasihi. Walimu wa kwanza wa Kiswahili kwa Walibora na waliomvutia zaidi bila kutanabahi ni babake na Kuto, kakake. Vinginevyo, sauti za walimu wa masomo mengine hazikumvutia kuyapenda wala kuyachangamkia.

**Sauti ya Mwalimu Kamatungu na Watibini**

Huyu alikuwa mwalimu wa hesabu na alimsababishia Walibora wingi wa machungu makalioni mwake kwa viboko vyake vya takriban kila siku kwa kuwa mwanachama wa kudumu katika orodha ya wapiga kelele darasani. Sauti ya mwalimu Kamatungu ni jazanda ya dhuluma dhidi ya mtoto. Viboko vya mwalimu huyo vilimfanya Walibora kubuni mbinu ya kuvikwepa kwa kufyatuka mbio hadi kiamboni mwao siku moja huku amefuatwa unyo unyo na Festo Makokha, mwanafunzi aliyekuwa mkimbiaji hodari shuleni. Kinaya ni kuwa badala ya Festo kumkamata Walibora na kumkabidhi mwalimu Kamatungu, alimhimiza kuzidisha mwendo ili asije akashikwa. Ni sauti iyo hiyo ya dhuluma iliyomfanya Walibora kupendelea kushiriki mazoezi ya riadha kila siku kwa wiki nzima kwenye uwanja wa shule ya msingi ya *Central* kuliko kuhudhuria masomo ya dhiki za viboko. Sauti ya viboko vya mwalimu ilimfanya Walibora kutopenda somo la hisabati na kuishia kupata alama duni katika mtihani wa kitaifa wa CPE.

Sauti ya mwalimu Watibini, aliyefunza somo la Kiingereza nayo ilikuwa ya kejeli. Licha ya kuzungumza Kiingereza kwa ung'ong'o, lafudhi ya Kibukusu haikumwambaa. Ni jazanda ya kejeli kwa sababu mwalimu huyo hakuweza kumfundisha Walibora kujua kusoma hicho Kiingereza, hadi mama yake mzazi alipojitolea kumfunza licha ya kuwa kisomo chake cha darasa la nne hakikumpa ujuzi wa mwalimu. Sauti ya mwalimu Watibini ni kinaya kwa utendakazi wa baadhi ya walimu katika shule za msingi nchini Kenya, kwamba, licha ya kuwa

na wanafunzi kwa siku tano kwa wiki, wanashindwa kuwafunza kumudu maarifa ya kimsingi kama kusoma. Walibora anakiri kufurahia zaidi vipindi walipokosa kufunzwa au walipoambiwa wakacheze uwanjani ilhali mwalimu wa kike akimfumia aidha mwanawe au mumewe fulana darasani. Hii ni sauti ya dhuluma dhidi ya haki ya watoto ya kupata elimu. Si ajabu kuwa Walibora hakutamani kuwa mwalimu licha ya kuwa na sauti nzuri wala baba aliyekuwa mwalimu mkuu.

**Sauti ya Mama**

Hii ndiyo sauti inayotawala na kupiga mwangwi riwaya nzima. Ni jazanda yenye maana pana na mchango mkubwa kwa hulka na falsafa za mwandishi Ken Walibora. Sauti ya mama ni mwalimu na mtetezi wa maadili ya upendo, uungwana na usamehevu. Walibora alipokokota nanga katika darasa la pili, mama alimliwaza kwa kumwambia kuwa alijua fika kuwa mwanawe si zumbukuku. Badala ya kumkaripia alimhimiza masomoni hadi akajitwika jukumu mwenyewe kumfunza jinsi ya kusoma. Sauti hii inafundisha zaidi kwa vitendo, kuliko ile ya baba iliyomfundisha Walibora Kiswahili kwa maneno na hotuba kwenye gwaride. Sauti ya mama pia ilimhimiza mtoto Walibora kukariri vifungu vya Biblia kama mazoezi ya kumudu stadi ya kusikiliza na kusoma Kiswahili. Mama alimfunza mwanawe kukariri Zaburi 146 kwa ukakamavu hadi akaikuza kumbukumbu yake. Mikarara hiyo ilimpa kujiamini kuwa alikuwa na chembechembe za kipawa cha utangazaji, kazi ambayo aliinukia kuifanya na kuipenda kwa dhati. Sauti ya mama inajenga jazanda ya mnato wa fasihi simulizi katika akili na hulka ya Walibora kama mhimili uliolinda uhai wake. Mwandishi anakiri kuchombezwa kwa sauti ya mamake alipougua na kupelekwa hospitalini Kitale. Alihisi maumivu makali makalioni kwa kudungwa sindano na tabibu. Mamake anasikika akimwimbia bembelezi ifuatayo:

*Olelo mulesi wa mwana,*
*Kona lilo mulesi wa mwana,*
*Mayi kecha, kecha ne nyama,*
*Olelo mulesi wa mwana*
(Walibora, 2014:14)

Kutokana na umuhimu aliouhusisha na fasihi simulizi ya kabila lake, Walibora alidinda kuutafsiri wimbo huo kwa kuhofia kuwa maana yake asili ingepotea. Kule kuhusisha bembelezi hiyo na mandhari ya hospitali ni thibitisho kuwa wimbo ni jazanda ya uhai wa fasihi simulizi ya Mwafrika katika ulimwengu unaolekea kumezwa na mawimbi ya utandawazi. Walibora amekuwa msitari wa mbele kuikuza na kuiendeleza fasihi ya Kiswahili ndani na nje ya Bara Afrika kwa kuifundisha vyuoni, kuitafitia, kuitunga na kuichapisha vitabuni, magazetini kwenye majarida na kwa mtandao.

Sauti ya mama ilisikika akilini mwa Walibora ikipinga kauli ya babu na baba kuwa Walibora atinwe kulingana na mila za Kibukusu. Sababu za kukataa mipango hiyo ya kutimiza mila ni kuwa kumrejesha mwanawe Baraki kungemletea mikosi iliyokuwa imepangwa na mahasimu wake ili kumsababishia mauko au kutokwa na damu bila kikomo au kutinwa visivyo. Njama hiyo ilitambuliwa na Nambuye, dadake Walibora. Sauti ya Nambuye inaungana na ya mama mzazi kumwepushia Walibora balaa. Sauti hizo mbili ni jazanda ya ukombozi. Zinamkomboa Walibora kutokana na mila angamivu na kumwachia mila za kuuhifadhi utu wake. Falsafa ya Walibora ni kudumisha mila zenye utu, undugu na ujamaa wa Kiafrika kwa makini ili mtu asije akasahu kuwa binadamu ni kigeugeu. Baada ya jando kukamilika, Walibora alifanyiwa sherehe kamili ya kutoka jandoni kama vile: kubeba mwenge wa moto, kulala mwituni na wanaume wenzake na kupewa mausia na wazee wake. Anaamini kuwa mwanamume si kutinwa kwa kisu cha ngariba tu, bali ni kujipatia kisomo chenye utu na maadili ya kujiwekea uungwana na mlahaka mwema na watu.

**Mwingilianomatini kati ya Jazanda za Wangari Maathai na Ken Walibora**

Katika nadharia ya semiotiki, hakuna matini isiyokuwa na mtagusano na matini nyingine katika fasihi. Mshabaha katika utunzi wa tawasifu upo kwa sababu za kifalsafa, kimazingira, kitamaduni, kijamii na kiuchumi. Ingawa Wangari Maathai aliishi katika mazingira yenye utamaduni tofauti na ule wa Walibora, jazanda wanazoteuwa kutumia katika tawasifu zao zina vipengele kadha vya mwingilianomatini. Kwanza, utamaduni wa jamiii za waandishi hawa unasawiriwa kuwa sehemu ya falsafa zao maishani. Wangari anazungumzia mandhari ya Mlima Kenya kama pumzi za uhai wake jinsi ambavyo Walibora anavyoyazungumzia mandhari ya Cherangani kulikoishi watu wa makabila tofauti. Kifalsafa, waandishi wawili hawa wanathamini utangamano wa makabila na watu wa tamaduni tofauti tofauti katika mazingira mamoja. Wanahubiri umoja na utangamano wa tamaduni mseto ili kuiunganisha jamii ya Kenya.

Pili, waandishi hawa wanateuwa jazanda za sauti ya fasihi simulizi ya jamii zao kuwa nembo ya kuzitambulisha nafsi zao. Wangari anasimulia ngano za wanyama kama chui walioishi kwenye mazingira yake na mtagusano uliokuwepo kati ya watu na wanyama mwitu. Walibora anawazungumzia wanyama wa pori kama swara aliozoea kuwawinda na vijana wenzake kama sehemu ya ukuaji wa mtoto wa kiume ila si kwa kitoweo. Wanyama mwitu wametumika kama jazanda ya kuwashajiisha na kuwakomaza Walibora na Maathai katika mazingira yao.

Tatu, sauti ya mama mzazi inatumiwa na waandishi hawa kuhubiri mafundisho kuhusu malezi mema yenye uchu wa kuisaka elimu ya shuleni bila kuchoka. Mamake Maathai anasikika akimhimiza sana bintiye kusoma kwa bidii shuleni. Mamake Walibora naye hamhimizi tu kwa maneno bali anajitolea kumfundisha mwanawe kumudu stadi ya kusoma na kukariri vifungu vya biblia.

Jazanda ya sauti ya mama kama mwalimu wa kwanza wa mtoto inakuzwa katika tawasifu za Maathai na Walibora. Nafasi ya mwanamke kama mzazi, mlezi na mwalimu inaitambulisha jamii ya Kiafrika.

Nne, Walibora na Maathai wanatumia mbinu ya jazanda kujieleza kwa mapana kuhusu tabia, matamanio, falsafa na ilhamu zao maishani. Kwa Walibora, sauti za bibi, baba, babu na mama zilichangia pakubwa kumwadilisha kuwa mpenda uungwana, usamehevu, utu na kutangamana na watu. Sauti hizo pia zilimfungulia ukurasa mpya maishani akajitambua yeye ni nani na ametunukiwa vipawa vipi. Himizo za sauti hizo zilimpa kujiamini na kuwa msomi, mwanahabari, mwandishi na mtetezi maarufu wa fasihi ya Kiswahili. Wangari Maathai kwa upande wake aliteuwa jazanda za miti na wanyama pori kuijenga tabia ya kuwa mkakamavu, mtetezi wa wanyoge, mwanamazingira, mpenda demokrasia na msomi mashuhuri. Sadfa ni kuwa waandishi hawa wanachangamkia taaluma zao kiasi cha kutoweza kubaini ikiwa ni vipawa walivyopewa na mungu au ni majaliwa kutokana na mazingira walimokulia. Sadfa nyingine ni kuwa wote ni wasomi watajika na wanataaluma waliopokea masomo yao nchini Kenya na Marekani.

Tofauti kubwa ya kifalsafa kati ya tawasifu ya Walibora na ile ya Maathai ni kuhusu mwamko wa kisiasa. Maathai ni mtetezi zaidi wa haki kuliko mila na desturi za Kiafrika. Hamuogopi yeyote yule anayetaka kumpokonya haki yake bali anaipigania kwa jino na ukucha, liwe liwalo. Tawasifu ya Maathai ni sauti ya ukombozi hasa wa mwanamke katika Karne ya Ishirini na Moja. Ken Walibora kwa upande wake anajitokeza kuwa mtu asiyevutiwa sana na msisimko wa kisiasa lakini mtetezi shupavu wa utu. Huenda sababu ikawa ni kipindi cha umri wake alichokisimulia. Masimulizi yake yanatujengea msingi wa usuli wake zaidi kuliko tabia na mienendo yake ya ukubwani. Usawiri huu wa falsafa unajitokeza kuwa mpaka mwembamba kati ya tawasifu na memwa.

Walibora ana upekee wake wa kimtindo kwenye matumizi ya mbinu za kweli-kinzani na tabaini. Katika mbinu hizi anaweka hali yakinifu sambamba na hali kanushi katika takriban matukio yote anayoyasimulia. Kwa mfano, ampigapo Kiberenge na kumuumiza kwa jiwe, anashangazwa na adhabu anayopewa na mamake badala ya kumsifu jinsi Daudi wa Biblia alivyosifiwa alipomuuwa Goliathi kwa manati. Pia anakariri uzumbukuku wake wa kutojua kusoma na kuandika ilhali alikuwa mwanawe mwalimu mkuu tena aliyefundisha somo la Kiswahili shuleni St. Joseph's. Hata tabia za bibi hazisazwi kwenye ulinganuzi huu; ana mazoea ya kukatiza masimulizi ya ngano kwa kuforota usingizini ila aamkapo hudai hajalala hata lepe. Mbinu hii inazitambulisha tungo za Walibora kama vile: *Nasikia Sauti ya mama; Siku Njema; Ndoto ya Almasi; Kufa Kuzikana; Mgomba Changaraweni; Mbaya Wetu; Fadhila za Punda; Kidagaa Kimemwozea* na mikusanyo yake mingi ya hadithi fupi. Kupitia mbinu hizi, Walibora anaeneza wazi falsafa yake kuwa mwanadamu ana sura mbili- chanya

na hasi. Sura hizi zinatokana na mifanyiko mingi ya kihistoria, kitamaduni, kijamii, kielimu na kisiasa. Mja sharti awe makini kuzipima sura zote mbili kwenye mizani ili kumwelewa mwanadamu barabara, kwa vile kukamilika si maumbile ya mtu.

## Hitimisho

Katika sura hii, nimetafsiri maana za baadhi ya jazanda alizotumia Wangari Maathai kujieleza kimaisha. Kupitia riwaya yake inayosawiri sifa za kitawasifu na kimemwa, mtunzi anadhihirisha usuli wake kwa ufahamu mkubwa wa mandhari alimolelewa na kukulia. Kwa uangalifu, mtunzi anatumia mbinu ya jazanda kusawiri falsafa na hulka zake kama mwanamke mkakamavu; mtetezi wa wanyonge, mlinda mazingira; na mwanasiasa mpenda haki. Kwa kutumia nadharia ya Semiotiki, mhakiki amepambanua ishara tofauti zilizotumika kuendeleza maudhui ya mtunzi wa riwaya. Kuna ishara za miti inayowakilisha tabia ya ukakamavu, utetetezi wa haki, uhifadhi wa mazingira, utetezi wa demokrasia, na muungano wa jamii. Pia mtunzi ametumia jazanda za kimaumbile kama vile jangwa la Sahara; mito Chania na Kanunga, Mlima Kenya na mabustani ya *The English Garden* na *Uhuru Park* kuonyesha falsfa yake ya kulinda na kuenzi mazingira. Watawala dhalimu wamesawiriwa kupitia jazanda za mazimwi ya Konyeki, mwanawe na Zimwi la Bustanini. Anachokienzi Maathai ni haki na usawa wa binadamu wote hasa wanyonge.

Walibora ametumia jazanda ya sauti kuangazia vyanzo vya maarifa, elimu na tabia zake hasa wakati alipokuwa mtoto. Sauti ni jazanda muhimu kwenye malezi yake, inayodhihirisha mila za Kiafrika kuwa mtoto daima alikuwa ni mpokezi wa makanyo, mafunzo, mila, tabia na falsafa kutoka kwa wakubwa wake nyumbani na shuleni. Anasimulia mafunzo aliyopata kupitia kwa sauti za mahirimu wa kike, bibi, babu, baba, mama, walimu naa mahasimu wake kama dira iliyomwelekeza na kuijenga tabia na falsafa yake maishani. Anasistiza haja ya utu na uungwana kama sifa inayomtenganisha amtu na mnyama. Tawasifu hizi mbili zimedhihirisha sifa za mwingilianomatini kupitia mbinu ya jazanda katika kuziunganisha jamii za Kenya kisiasa na kitamaduni.

## Marejeleo

Alabi, I. A. (1998). *Continuities and Divergences in Black Autobiographies of Africa and the Diaspora.* Doctoral Thesis. Canada: University of Saskatchewan.

Bengtsson, M. L., Ovessen, R., & Fity, E. (2008). *Wangari Maathai: Unbowed, A Memoir. The analyses of the ideological vision of a contemporary Kenyan woman.*

Eagleton T. C. (1996). *Literary Theory: An Introduction* (2nd Ed.). Minnesota: The University of Minnesota Press.

Maathai, W. (2007). *Unbowed, A Memoir*. London: Arrow Books.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es salaam: Mture Educational Publishers.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Wafula R. M., na Njogu, K. (2007). *Naaharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K. (2014). *Nasikia Sauti ya Mama*. Nairobi: Longhorn.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wamitila, K. W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele yake*. Nairobi: Phoenix.

Smith, S., & Watson, J. (1992). 'De/Colonizing and the Politics of Discourse in Women's Autobiographical Practices.' In Smith, S. & Watson, J. (Eds). *De/Colonizing the Subject: The Politics of Gender in Women's Autobiography. Pp. xiii-xxxi* Minneapolis: University of Minnesota Press.